HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

SHULE YA SEKONDARI ITALA,
S.L.P. 1252,
MBEYA

KUMB NA. ITLSS/T.1SEL/…… 05/12/2020.
MWANAFUNZI……
S.L.P……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2021

1. Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Itala mwaka **2021.** Shule ipo umbali wa km 45 mashariki mwa mji mkuu mkoa wa Mbeya. Usafiri wa basi kutoka mbeya mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Uyole

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** saa moja asubuhi.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

(A) Suruali mbili moja rangi ya damu ya mzee na nyingine rangi ya bluu bahari
(B) Mashati meupe mawili kitambaa cha Tetron
(C) Tisheti ya zambarau na track suti ya bluu bahari
(D) Viatu vyeusi vyenye kamba na soksi nyeusi jozi mbili
(E) Sweta mbili rangi ya damu ya mzee

(ii) **Wasichana**

(A)Sketi mbili moja rangi ya damu ya mzee na nyinginge rangi ya bluu bahari
(B)Mashati meupe mawili kitambaa cha Tetron
(C)Tisheti ya zambarau na track suti ya bluu bahari
(D)Viatu vyeusi vyenye kamba visivyo na visigino virefu na soksi nyeupe jozi mbili
(E)Sweta mbili rangi ya damu ya mzee

(iii**) Sare za michezo**

(A) Bukta ya bluu na tisheti ya bluu ambayo ina nembo ya TANZANIA
(B) Daruga au raba za michezo

3.0 SHERIA ZA SHULE

3.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na – 75 ya mwaka 1978.aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya elimu nchini.
Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo

.Heshima kwa walimu,viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

.Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

.Kutimiza kwa makini maandalio ya join(preparation) kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa

.Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii

.Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule

.Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

.kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

3.**2 Makosa yafuatayo yaweza kusababisha ufukuzwe shule**

1. Wizi
2. Uasherati,Ubakaji na Ushoga
3. Ulwvi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
8. Kudharau bendera ya Taifa
9. Kuoa au Kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya Shule
11. Kutoa mimba
12 .Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu
13. Kukataa adhabu kwa makusudi

KARIBUNI SANA SHULE YA SEKONDARI ITALA

…….
HELENA J. KAMWELA
MKUU WA SHULE

FORM (REQUEST FOR MEDICAL EXARMINATION THIS FORM IS TO BE COMPLETED BY A MEDICAL OFFICER

Name of student …….

Age……. Sex……

The above named has been examination is respect of:

a) STOOL :……

b) URINE : …….....

c) CHEST : ……...

d) BLOOD : …….

e) EYES : …….

f) EARS : …….

g) OTHER FINDINGS ; ……..

……...

……

I am satisfied that above named student is fit/not fit to pursue further studies in a secondary school.

…….. ……

SIGNATURE DATE

…….. ……...

DESIGNATION STATION

NB: Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi katika sehemu yake pamoja na Mwanafunzi katika sehemu yake na halafu irudishwe shuleni pamoja na Picha nne (passportsize) za mwanafunzi.

Mimi …….. Mzazi/Mlezi wa mtoto

Wangu ……... nimesoma, nimeelewa na Nimekubali masharti yote yanayohusu mtoto wangu kuingia shule ya sekondari Itala. Nitampa Mahitaji yote yanayotakiwa na nitashirikiana na Walimu wa shule ya sekondari Itala katika kumlea Vizuri mtoto wangu ili apate kunufaika na elimu atakayoipata hapa Shuleni.

Saini ya mzazi/mlezi……..

Anuani ya mzazi/mlezi …….
……
……

Namba ya simu ……

Mimi …….....mwanafunzi naelewa Ni dhamana kubwa sana kwangu kupatiwa nafasi katika shule ya Serikali. Naahidi kutii sheria za shule na nitajitahidi kuwa Mwanafunzi mwema na mwenye bidii na mwenye nidhamu katika kazi zote za darasani na kazi za mikono kwa muda wote nitakaposoma katika shule ya sekondari Itala. Sitashiriki katika vikundi viovu au migomo au maasi ya aina yoyote. Naahidi daima nitaweka Moyo wa ujasiri na wa kizalendo mbele, utovu wa nidhamu kwangu itakuwa mwiko.

Saini ya mwanafunzi……

Tarehe ……